# Mustakabali wa misaada kwa wakulima wadogo nchini Tanzania:



## Tunaelekea wapi baada ya Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku?

**MUKHTASARI**

Septemba 2018

african centre for biodiversity
www.acbio.org.za

# Contents

Vifupisho 3
Utangulizi 4
Kuandaa njia kwa programu za ruzuku za pembejeo nchini Tanzania 4
Mfumo Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku na athari zake kwa wakulima wadogo 5
Kutathmini Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku 7
Mustakabali wa ruzuku za pembejeo nchini Tanzania 8
Marejeo 12



Mnamo Aprili 7, 2015, Kituo cha Afrika cha Usalama wa Kibaiolojia kilibadilisha jina lake rasmi na kuitwa Kituo cha Africa cha Bioanuwai (ACB). Mabadiiko haya ya jina yalikubaliwa kupitia mashauriano ndani ya ACB ili yaakisi kupanuka kwa wigo wa kazi yetu katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Machapisho yote ya Kituo cha Africka cha Bionuwai kabla ya tarehe hii yatanbaki chini ya jina la zamani la Kituo cha Afrika cha Usalama wa Kibaiolojia, na yanapaswa kuendelea kutumika kama rejea kwa jina hilo.

Dhamira yetu imeendelea kuwa kubomoa ukosefu wa usawa katika mifumo ya chakula na kilimo barani Afrika na tunaamini katika haki za watu za kupata chakula chenye lishe na stahiki kitamaduni, kilichozalishwa kupitia njia zilizo sahihi kiekolojia na endelevu, na haki yao ya kuainisha mifumo yao wenyewe ya chakula na kilimo.

© Kituo cha Afika cha Bioanuwai cha Afrika

www.acbio.org.za
S.L.P. 29170, Melville 2109, Johannesburg, Afrika Kusini. Simu: +27 (0)11 486 1156

Timu ya Utafiti: Linzi Lewis na Sabrina Masinjila, Kituo cha Africa cha Bioanuwai
Picha ya Jalada: Lisolomzi Pikoli
Mhariri nakala: Liz Sparg
Ubunifu na mpangilio: Adam Rumball, Sharkbuoys Designs, Johannesburg

## Shukrani

Shukrani zetu kwa wakulima na wale walioshiriki katika utafiti huu, kwa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), na kwa Stephen Greenberg na Mariam Mayet kutoka Kituo cha Afrika cha Bioanuwai, kwa michango yao na msaada. Aidha, Kituo cha Afrika cha Bioanuwai kinatoa shukrani kwa msaada mkubwa wa Shirika la Uswisi la Maendeleo na Ushirikiano (SDC). Maoni na mawazo yaliyotolewa katika ripoti hii ni ya Kituo cha Africa cha Bioanuwai na si lazima yaakisi sera rasmi au msimamo wa wafadhili wetu.

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ACB | Kituo cha Africa cha Bioanuwai |
| AGRA | Muungano wa Mapinduzi ya Kijani barani Africa |
| AFSP | Programu ya Haraka ya Usalama wa Chakula |
| DAP | Mbolea ya DAP yenye Diammonium fosfeti |
| FAO | Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo |
| FISP | Programu ya Ruzuku za Pembejeo za Kilimo |
| IDA | Taasisi ya Maendeleo ya Kimataifa |
| MAFC | Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika |
| MVIWATA | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| NAIVS | Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku |
| OPV | Mbegu Bora Zilizochavushwa Kiasili |
| PELUM | Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi Kiekolojia |
| QDS | Mbegu Zilizothibitishwa Ubora |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika |



# Utangulizi

Huu ni muhtasari wa ripoti kamili inaozungumzia kuhusu 'Mustakabali wa misaada kwa wakulima wadogo nchini Tanzania: Tunaelekea wapi baada ya Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku?" uliofanyiwa utafiti na Kituo cha Afrika cha Bionuwai (ACB). Ripoti hii inajadili ruzuku za pembejeo za kilimo nchini Tanzania, ikiangazia athari zake kwa wakulima wadogo, na kujikita hasa katika Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za pembejeo ya ruzuku. Programu za Ruzuku za Pembejeo za Kilimo unalenga kuwezesha matumizi ya pembejeo za kilimo ili kuongeza tija kwenye kilimo na kwa sehemu kubwa inawalenga wakulima wadogo. Mfumo wa Kitaifa wa **Vocha za Pembejeo ya ruzuku**, programu kubwa ya Ruzuku za Pembejeo za Kilimo Tanzania, ilijikita kwenye ugavi wa mbegu bora za mahindi, mpunga na mbolea ya viwandani kupitia usambazaji wa vocha kwa wakulima wadogo. Mradi wa Mfumo wa Kitaifa wa **Vocha za Pembejeo ya ruzuku** uliendeshwa kwa miaka mitano, pamoja na juhudi za Serikali za kuendeleza mfumo huo baada ya hapo. Lakini jambo hili lilikwamishwa na bajeti finyu na udhaifu wa kiufanisi katika utekelezaji. Ripoti hii inalenga kuchangia katika majadiliano kuhusu aina ya misaada ambayo inaweza kutolewa kwa wakulima wadogo ili kuhimiza kilimo anuwai ambacho ni endelevu zaidi, kilimo cha kijamii na kiekolojia, na kinachojumuisha mahitaji ya makundi mbalimbali ya wakulima wadogo.

Muhtasari huu unagusa vipengele muhimu vya ripoti kuu ikijumuisha historia fupi kuhusu kuandaa njia kwa ajili ya programu za ruzuku za pembejeo nchini Tanzania, Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku na athari zake kwa wakulima wadogo, tathmini ya Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku na programu za ugavi wa pembejeo; na mustakabali wa ruzuku za pembejeo nchini Tanzania.

# Kuandaa njia kwa programu za ruzuku za pembejeo nchini Tanzania

Tangu janga la njaa la chakula duniani wa mwaka 2007/08, ambao ulishuhudia kuongezeka kwa kasi kwa bei za vyakula na matokeo yake ya kuongezeka kwa kukosekana kwa usalama wa chakula na umasikini vijijini, dunia imeshuhudia msisitizo mpya kwenye programu za kusaidia uzalishaji wa kilimo. Katika baadhi ya nchi za Kiafrika kama vile Malawi, Zambia, Ghana na Tanzania, pembejeo zilizopewa ruzuku kwa wakulima wadogo ni sehemu muhimu ya kuwasaidia wakulima. Programu hizi za ruzuku za pembejeo za kilimo hutumia sehemu kubwa ya bajeti za kilimo, huku nchi 10 za Afrika zikiwa zimetumia takribani Dola za Marekani bilioni 1 kwenye programu hizi kati ya mwaka 2000 na 2011, ikiwa karibu asilimia 30 ya bajeti zao za kilimo kwa wastani (ACB, 2016).

Ruzuku zinalenga kuwezesha matumizi makubwa ya pembejeo, na hasa kwenye mbegu na mbolea za viwandani, kuongeza uzalishaji wa kilimo, hususani wa mazao ya chakula kikuu kinachotumiwa na wananchi. Ushahidi unapendekeza kwamba ijapokuwa mavuno ya vyakula vikuu kama vile mahindi yameongezeka kwa wastani katika baadhi ya maeneo, programu za ruzuku ni ghali sana na sio endelevu baada ya muda mrefu (IAPRI, 2017; Jayne et al, 2018). Kuna nyaraka nyingi zinazoonyesha wasiwasi mkubwa, ikijumuisha gharama kubwa za utawala, matokeo finyu kwenye umasikini na maisha ya watu, mwelekeo wa kuwanufaisha wale ambao tayari wako vizuri kiuchumi, upendeleo wa kisiasa, kitabaka na rushwa; makampuni makubwa kudhibiti mnyororo wa thamani wa pembejeo za kilimo, na upotoshaji wa masoko ya kilimo. Kuendelezwa kwake kwa sehemu kubwa kunatokana na matumizi yake kama chombo cha kuunga mkono kisiasa.

Programu ya Ruzuku za Pembejeo za Kilimo zimebuniwa kwa sehemu ndogo kutatua masuala ya usalama wa chakula na lishe kupitia mbinu zinazoelekezwa sokoni kama

vile kujumuishwa kwenye minyororo ya thamani ya kibiashara, ambayo huelekea kuweka msisitizo kwenye vyakula vichache, vinavyotumiwa na wengi na vilivyojaa kalori. Makampuni makubwa ya kimataifa ya mbegu, mbolea na kemikali za kilimo ni wanufaika wakuu, kwa vile hupata masoko ya uhakika kutokana na ruzuku zitolewazo kwa umma. Wakati kikundi kidogo cha wakulima kinaweza kunufaika, wengi kati ya wakulima masikini walio na uwezo mdogo wanakuwa tegemezi kwenye pembejeo zenye ruzuku. Kuliko kujenga kwenye mtaji wa kijamii katika jamii za wakulima wadogo masikini walio na rasilimali chache, programu hizi kutoka nje zinazolazimisha suluhisho moja kwa kila tatizo, hugandamiza mbinu anuwai za kuwasaidia wakulima wadogo kujenga na kuimarisha mifumo yao ya asili ya mbegu na kilimo.

Programu za Ruzuku za Pembejeo za Kilimo zilikuwa maarufu katika nchi kadhaa za Africa chini ya Sahara kabla ya miaka ya 1970 hadi zilipoondolewa kwenye miaka ya 1980, kutokana na kuporomoka kwa uchumi ambayo ilipelekea programu za marekebisho ya miundo. Nchini Tanzania, baada ya muongo mmoja bila ya ruzuku za pembejeo, zilianzishwa tena mwaka 2003/04 katika mfumo wa ruzuku zilizohusisha gharama za usafiri na sehemu ya gharama za bei ya mlaji, na sehemu ya gharama za mtumiaji wa mbolea (Cagley et al., 2009). Serikali iliingia katika mikataba ya makubaliano na makampuni kusambaza mbolea ambayo hatimaye ilisambazwa kwa wakulima kwa gharama iliyokubaliwa na Serikali na makampuni (URT, 2012b). Ruzuku hii hatimaye iliondolewa kwa sababu wa wasiwasi kuhusu kutokuwa na ufanisi, manufaa yasiyolingana na gharama, kulenga na kusambaza faida na badala yake Ruzuku inayotokana na vocha, Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku, ukachukua mahali pake.

Ruzuku za pembejeo ni sehemu tu ya misaada ya Serikali kwa wakulima wadogo. Hata hivyo, ni kipengele muhimu kwa vile kinaunda kwa kiasi kikubwa mbinu za uzalishaji na mielekeo kuhusiana na usimamizi wa mbegu, udongo na udhibiti wa wadudu waharibifu. Kama zilivyoundwa kwa sasa, Programu za Ruzuku za Pembejeo za Kilimo huelekeza msaada wa sekta ya umma kwenda njia ya Mapinduzi ya Kijani. Kuna maridhiano yanayokithiri duniani kwamba utendaji wa uzalishaji ulio anuwai, endelevu kijamii na kiekolojia, ni muhimu kwa mustakabali wa kilimo. Ripoti hii inaitazama Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku na athari zake kwa misaada kwa mkulima katika muktadha wa mabadiliko ya tabia nchi, kuongezeka ukosefu wa usawa, na mmomonyoko wa msingi wa rasilimali asilia katika mfumo wa kupungua kwa rutuba ya udongo, uchafuzi wa maji na kupotea kwa bioanuwai ya kilimo.

## Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku na athari zake kwa wakulima wadogo

Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku ulikuwa kipengele kikubwa zaidi cha Programu ya Haraka ya Usalama wa Chakula, ambayo ilijadiliwa baina ya Serikali na Benki ya Dunia na kuzinduliwa mwaka 2009. Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku ulianzishwa ili kubadili na kuondoa mapungufu ya programu iliyopita ya ruzuku ya usafirishaji wa mbolea. Kauli ya msingi ya mfumo wa ruzuku ya vocha ni matumizi ya vocha kwa baadhi ya wakulima waliochaguliwa kununua pembejeo (kwa ujumla mbolea na mbegu) kwa bei yenye ruzuku. Hivyo mgavi wa pembejeo hubadili vocha kwa pesa taslimu kutoka kwa Serikali, au taasisi ya fedha yenye mahusiano na progrmu ya ruzuku. Kifurushi hiki kwa kinajumuisha vocha 3: kilo 10 za mbegu za mahindi – ama  Mbegu Zilizochavushwa Kiasili (OPV) au mahindi chotara – au kilo 15 za mbegu za mpunga, ambazo kwa ujumla zinatosha kwa hekta moja ya shamba. Kati ya vocha, asilimia 80 zilipangwa kwa wakulima wa mahindi, wakati asilimia 20 zilizobaki zilitolewa mbegu za mpunga. Vocha ya pili ilikuwa kwa ajili ya mbolea ya msingi, ama kilo 150 za diammonium phosphate (DAP) au mifuko miwili ya kilo hamsini hamsini ya Fosfeti ya Mwamba ya Minjingu, na Vocha ya tatu ni kwa ajili ya mbolea ya kukuzia, kwa ujumla kilo 50 za Urea (Pan and Christiaensen, 2012).



Mfumo wa Vocha kwa mara ya kwanza ulifanyiwa majaribio katika wilaya mbili za mikoa ya Mbeya na Rukwa mwaka 2007/8. Hii baadaye ilipanuliwa hadi wilaya 58 katika mikoa 11 iliyoonyesha uwezo – haya ni maeneo yaliyo na uzalishaji mkubwa wa mahindi yenye hali ya hewa, udongo unaofaa, n.k. – mwaka 2008/9,[1] na kwenye maeneo ambako wakulima wa mpunga wanaweza kufanya umwagiliaji. Hatimaye ilikuwa programu ya kitaifa (Benki ya Dunia, 2014b). Lengo la muda mfupi ilikuwa kuongeza mara moja uzalishaji wa chakula. Uchaguzi wa walengwa na kuanzisha wasambazaji wa pembejeo za kilimo wa kusambaza pembejeo katika ngazi ya kijiji ulibuniwa ukiwa na lengo la muda mrefu la kuanzisha mfumo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo unaosukumwa na soko (Mather and Ndyetabula, 2016). Mfumo huu uliogatuliwa wa usambazaji wa vocha za pembejeo ulilenga katika kupanua uzalishaji wa mahindi na mpunga ili kuboresha uhakika wa chakula wa kaya na taifa, katika kujibu kuongezeka haraka katika bei za nafaka na mbolea mwaka 2007 na 2008, ikiambatana na ukame na kuongezeka kwa bei za chakula (URT, 2014a; Pan and Christiaensen, 2012). Malengo mengine yalikuwa ni kuanzisha na kuongeza ufikiwaji na upatikanaji wa mbegu bora za mahindi na mpunga, na kuimarisha minyonyoro ya ugavi wa pembejeo kwa mbegu bora na mbolea kupitia wasambazaji pembejeo wanaofahamika (Benki ya Dunia, 2014b).

Mnamo 2007/8, Muungano wa Mapinduzi ya Kijani barani Africa (AGRA), kwa kushirikiana na Wizaraya Kilimo, Chakula na Ushirika ilifadhili mafunzo ya wasambazaji pembejeo katika halmashauri za wilaya 14. Ufadhili wa Benki ya Dunia ulijumuisha ufadhili kwa ajili ya mafunzo ya wasambazaji 3,855 ambao walisajiliwa kushiriki katika programu hii, ambayo ilifanyika kabla ya msimu wa usambazaji wa pembejeo wa mwaka 2009/2010. Kati ya hawa, wasambazaji wa pembejeo 2,010 walibaki amilifu katika usambazaji wa pembejeo za kilimo. (Benki ya Benki, 2014b).

Katika bajeti iliyopangwa kwa ajili ya Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku ilikuwa kati ya Dola za Marekani Milioni 60 na Milioni 100 kwa mwaka, kati ya asilimia 8.4 na 33 ya jumla ya bajeti ya kilimo, kutegemeana na ufadhili, idadi za vocha zilizosambazwa, kubadilika kwa kila mwaka kwa gharama za mbolea inayoingizwa nchini (Benki ya Dunia, 2014b). Wakati wa miaka miwili ya mwanzo ya mradi, Taasisi ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA)[2] ilifadhili asilimia 50 ya gharama za ruzuku, wakati asilimia 50 iliyobaki ilifadhiliwa na Serikali. Kutokana na ucheleweshaji mkubwa wa fedha za serikali, taasisi ya IDA iliongeza mchango wake hadi asilimia 83 kwa msimu wa kilimo wa 2010/11 (Benki ya Benki, 2014b). Ufadhili kutoka nje taratibu ukapungua katika kipindi cha utekelezaji, na hatimaye ukasitishwa mnamo 2013/14, na kuzuia uwezo wa Serikali kuendelea kutekeleza hii programu (Cameron et al, 2017). Serikali iliendelea kutoa ruzuku mwaka 2014/15 hadi 2016/17 kupitia mbinu tofauti, ikibadilia aina ya ruzuku, ikijumuisha ruzuku zitokanazo na mkopo, kwa kutoa mikopo kwa vikundi vya wakulima na ushirika kupata pembejeo; matumizi ya vocha kwa msimu mmoja; na kuingia mikataba na makampuni ya mbegu na mbolea ili kusambaza pembejeo za mbegu na mbolea. Baada ya hapo Serikali peke yake ikafadhili programu ya ruzuku, kiasi ambacho kilipunguzwa katika bajeti ya mwaka 2016/17, ikionyesha kwamba fedha itakayotolewa itakoma kwa siku zijazo (Cameron et al, 2017).

Katika hotuba ya bajeti ya 2017/18 Serikali ilithibitisha kwamba itaendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya mbegu za mahindi na mpunga, na mbolea kupitia mikataba na makampuni. Kuimarishwa kwa manunuzi ya mbolea kunaonekana kama njia yenye manufaa yanayolingana na gharama, kupitia Kanuni za Mbolea (Ununuzi kwa Wingi) za mwaka 2017[3] (kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Mbolea ya

1. Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa katika nyanda za juu kusini; na Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Kigoma, Tabora, Mara na Morogoro katika maeneo ya katikati na kaskazini mwa nchi. Pwani iliongezwa mwaka 2009/10.
2. Taasisi ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA) ni taasisi ya fedha ya kimataifa ambayo hutoa mikopo na ruzuku zenye masharti nafuu kwa nchi zinazoendelea zilizo masikini sana. Kwa pamoja, Taasisi ya Maendeleo ya Kimataifa na Benki ya Kimataifa ya Ukarabati na Maendeleo kwa ujumla hujulikana kama Benki ya Dunia.
3. Angalia Kanuni za Mbolea (Ununuzi kwa Wingi) za mwaka 2017, Notisi ya Serikali Na. 49, Toleo Na. 7,17 Februari 2017.

mwaka 2009) kwa aina mbili za mbolea, Urea na DAP. Lengo ni kufanya mnyororo wa ugavi wa pembejeo kuwa shindanishi zaidi, hasa kwa DAP na Urea ambapo maoni ni kwamba makampuni ya ndani yanaweza kushiriki katika kufanya masoko na usambazaji. Serikali imekadiria kwamba hili litasababisha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini.

## Kufanya Tathmini ya Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku na programu za ugavi wa pembejeo

Ukosefu wa ufanisi katika utoaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku umeripotiwa katika tafiti nyingi, kujumuisha: kuchelewesha katika utoaji wa vocha na pembejeo, matumizi mabaya ya vocha; kutokuwepo kwa ufahamu sahihi miongoni mwa wakulima wadogo kuhusu njia ambazo program hufanya kazi. Kuchelewa kwa utoaji huduma husababisha ucheleweshaji katika kupanda mazao na ndio lilikuwa lalamiko kubwa la wakulima. Katika baadhi ya matukio, kama vile mwaka 2011/12, pembejeo ziliwasili tayari kwenye msimu wa mvua. (Benki ya Dunia, 2014b). Wakulima ama hawakuweza kupanda au walipanda mbegu za asili badala yake (REPOA, 2017). Pembejeo zilipocheleweshwa, wakulima bado walitakiwa kununua kifurushi kizima.

Wakulima sio tu wanakuwa tegemezi katika kutumia mbegu bora za mahindi na mpunga na mbolea za viwandani, lakini pia badala yake wanategemea ugavi unaoendelea wa pembejeo zenye ruzuku (Benki ya Dunia, 2014b). Gharama zinazoongezeka za pembejeo za mbegu bora na kemikali zinapunguza kiwango cha faida, na kuna uwezekano wakulima wakadai kuendelea na kupanuka kwa ruzuku pasipo mwisho, au upatikanaji wa mikopo nafuu (IPES-Food, 2017).

Pia kuna ripoti zinazotofautiana za rushwa na kuvuja, changamoto katika uchaguzi wa walengwa na wasambazaji wa pembejeo. Walengwa hatimaye walichaguliwa na Kamati za Kijiji za Vocha na Mabaraza ya Kijiji, pakiwa na madai ya uchaguzi usio wa haki na upendeleo ulioonyeshwa na viongozi wa kitongoji.[4] Kilicho wazi ni kwamba, wale waliokuwa na jukumu la kuchagua walengwa walikuwa na ushawishi mkubwa juu ya ugawaji wa vocha, na uwezekano wa matokeo yake kuwa na ufadhili wa kisiasa, rushwa na upendeleo (DANIDA, 2012). Katika matukio machache, wakulima waliuza vocha, kutokana na uwezo wao mdogo wa kumudu pesa ya kuongezea, (na wakati mwingine wana mahitaji ya pesa ya kununulia chakula), hawataki kuchukua kifurushi kizima, au pale pembejeo zinapochelewa. Katika baadhi ya matukio, wakulima waliambiwa watie saini kwa vocha zote lakini walishindwa kupokea pembejeo zao zote (Benki ya Dunia, 2014b). Wasambazaji wa pembejeo walichaguliwa na makampuni ya mbegu/mbolea, badala ya wana vijiji, jambo linalofanya iwe vigumu kuwawajibisha inapotokea utendaji mbovu (REPOA, 2017).

Kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku , wakulima walielekezwa katika uzalishaji wa mahindi chotara, hata katika mazingira ya uhaba wa mvua, ikiwa na athari za muda mrefu za kupunguza uanuwai wa kilimo, na chakula kidogo kupatikana vijijini. Mhamo kuelekea mahindi chotara ya kiwango kilichokubalika na aina bora za mpunga zilibadili aina za mbegu za kienyeji, ambazo mara nyingi zilipendwa katika masoko ya wenyeji. Katika maeneo haya, wakulima walipendelea kupanda mbegu chotara kwa ajili ya kuuzia masoko ya viwandani, wakati wakipendelea aina za kienyeji kwa matumizi yao. Matumizi ya muda mrefu ya mbegu chotara na aina za mbegu zilizotayarishwa kwa ajili ya mnyororo wa thamani wa biashara (kwa mfano, kwa ajili ya matumizi kama pembejeo katika uzalishaji wa chakula cha mifugo kiwandani) ikiambatana na vifurushi vya mbolea ya viwandani ya kiwango kilichokubalika, zina athari hasi kwenye afya ya ekolojia na udongo, pia hupunguza uanuwai wa chakula

4. Kitongoji ni sehemu ndogo ya kijiji kiutawala nchini Tanzania. Kwa kawaida vitongoji 3 – 5 hufanya kijiji.

na usalama wa lishe (ACB, 2016b). Japokuwa kuongezeka kwa mavuno kunatarajiwa kwenye mikondo ya soko kuchukua chakula za ziada, masoko ya kibiashara hayapatikani kwa wakulima wengi. Matokeo yake ni aina za vyakula visivyostahili kufurika masoko ya wenyeji. Sehemu kubwa ya motisha na uhalalishaji wa kuweka mkazo kwenye mazao machache yanayolipa kibiashara katika Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku lazima uhojiwe, hasa pale ambapo masoko ya wenyeji yanaposhindwa kununua nafaka za ziada, na wakati ukosefu wa uhakika wa chakula ukiendelea.

Kuelekeza rasilimali za wenyeji kwenye mbegu za kibiashara na mbolea za viwandani kutoka nje zinazoendelea kuwa ghali zaidi, kunaleta wasiwasi mkubwa pale ambapo wakulima hawawezi tena kupata mbegu za kienyeji ambazo zinahudumia kama mkakati[5] wa kupunguza hatari. Kuna wakulima ambao bado wanazalisha mbegu za asili, ambazo zina uhitaji mkubwa. Ijapokuwa hiki ndio chanzo pekee cha mbegu kwa mazao mengi, wakulima hawa kwa sasa hufanya shughuli zao pembezoni, na hutengwa zaidi na sheria za mbegu za kibiashara ambazo zinataka kumzuia mkulima kutumia na kubadilishana mbegu.

## Mustakabali wa ruzuku za pembejeo nchini Tanzania

Wakati mustakabali wa ruzuku za pembejeo nchini Tanzania ukiwa haueleweki, tunaakisi kwenye changamoto na uwezekano kuhusu mustabali wa kutengwa kwa rasilimali finyu za umma  Kilicho wazi  ni kwamba kuendelea kwa Serikali kusaidia wakulima wadogo ni muhimu ili kukidhi Ajenda ya Dunia 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).[6] Hususani Lengo Na. 2 ambalo linalenga “kutokomeza njaa, kufikia uhakika wa chakula na kuboresha lishe na kukuza kilimo endelevu.’.

Tukiangalia programu ya Mfumo wa Kitaifa wa Vocha za Pembejeo ya ruzuku, maswali mengi yanabaki. Je, Wizara ya Kilimo iwekeze asilimia 30 – 40 ya bajeti yake ya mwaka katika ruzuku za pembejeo, au kiasi hiki kitawekezwa vizuri zaidi kupitia kuanuwai na kuimarisha mifumo mingine ya msaada”? Je, ruzuku ziwahudumie wakulima wenye uwezo mkubwa wa rasilimali, au zijumuishe wale walio na rasilimali  chache na wanaoishi katika mazingira pembezoni zaidi? Je, ruzuku kimsingi zinufaishe makampuni binafsi ya kigeni ya mbegu na kemikali za kilimo? kuendeleza minyororo ya ugavi wa pembejeo, au msisitizo uwe kwenye kuimarisha na kusaidia masoko ya ndani, kulingana na uzalishaji anuwai wa mbegu na mazao na wakulima wenyewe? Je, ni pembejeo gani zilizo endelevu zaidi za kilimo-ekolojia na mbinu zake ambazo zinaweza kufikiriwa kwa ajili ya ruzuku?

Wakulima wadogo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali na zinazoingiliana. Kushughulikia yote haya, mkusanyiko wa msaada mahususi inaweza kufanywa na Serikali, mashirika ya wakulima na asasi za kiraia na wadau wengine. Hususani, kuna haja ya kuwa na majadiliano juu ya maboresho ya ajenda ya sasa ya Mapinduzi ya Kijani, hasa kwa vigezo vya kuhamisha rasilimali kuelekea kwenye kilimo–ekolojia. Maboresho yanaweza kujumuisha ubunifu jumuishi na msaada kwenye mbegu, udongo na maji, kama vile:

- Kukuza mabaki ya viumbe hai kwenye udongo kupitia matumizi ya mbolea hai, mboji, mbolea ya ng’ombe na kuku, mbolea ya chai, kilimo-misitu;
- Kutambua, kukuza, kusaidia na usambazaji wa mbegu za wenyeji na za asili kupitia maonyesho ya mbegu, tamasha la mbegu, kubadilishana mbegu;
- Kuingiza mbegu za kienyeji na asili kama sehemu ya kifurushi cha Programu ya Ruzuku za Pembejeo za Kilimo;
- Hifadhi ya maji kupitia kukuza umwagiliaji na teknolojia za kuvuna maji, kama vile visima, mito na mabwawa;
- Uzalishaji jumuishi wa mazao, mifugo, kilimo-misitu kupitia dawa za kilimo hai za

5. Majadiliano ya vikundi vya wakulima, August 2017
6. Angalia Malengo ya Maendeleo Endelevu: Malengo 17 ya kubadili ulimwengu wetu https://www.un.org/sustainabledevelopment/sustainable-development-goals/

kuua wadudu waharibifu kwenye bustani;
- Kukuza masoko ya ndani ya chakula ambayo yanasaidia vyakula vizima vya wenyeji, vyenye lishe na;
- Kushughulikia vipengele vya kijamii na kiuchumi vya kilimo-ekolojia ikijumuisha wanawake, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, maji na kilimo, chakula, mbegu na haki za ardhi
- Motisha wa moja kwa moja kutoka Programu ya Ruzuku za Pembejeo za Kilimo kwenda kwa wakulima wa kujitegemea wanaotumia mbinu za kilimo-ekolojia unaofaa kwa maeneo yao;
- Kujenga harakati na ufahamu na kampeni kuhusu kilimo-ekolojia kuanzia ngazi za kijiji hadi mkoani;
- Kilimo-ekolojia kinachotokana na ushahidi kama mbadala wa Programu ya Ruzuku za Pembejeo za Kilimo za sasa, kushirikishana maarifa ya wenyeji kuhusu thamani ya mbegu;
- Mafunzo ya mkulima kwa mkulima na ziara za kubadilishana uzoefu;
- Vituo vya wenyeji vya kilimo-ekolojia;
- Kushiriki sera na midahalo na watunga sera katika ngazi zote.

Kilimo-ekolojia kinaweza kuchangia katika kukidhi malengo mengi mahususi ya Lengo Na. 2 la Maendeleo Endelevu, kwani inawakilisha mifumo endelevu ya uzalishaji wa chakula na utendaji endelevu wa uzalishaji wa chakula ambao unaongeza tija na uzalishaji; husaidia kuendeleza mifumo ya ekolojia; kuimarisha uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, hali ya hewa mbaya, ukame, mafuriko na majanga mengine, na taratibu huboresha ardhi na ubora wa udongo (Lim, 2018). Kuna historia ndefu ya utafiti linganifu inayoonyesha ustahimilivu wa ***utendaji wa kilimo-ekolojia***, na uwezo wake wa kufanya vizuri zaidi ya kilimo cha kawaida kwenye viashiria mbalimbali, hususani wakati wa ukame (IAASTD, 2009; Rodale Institute, 2011; IPES-Food 2016). Nyingi katika mbinu hizi kama vile kutandaza majani kwenye mashina au kilimo mseto hazina gharama kubwa, ni rahisi na hazina athari za kiafya.

Wajibu wa utafiti na ugani ni muhimu katika kuwa na Programu anuwai za Ruzuku za Pembejeo za Kilimo kwa kuelekeza msaada kwenye utendaji wa kilimo-ekolojia. Kwa bahati mbaya, mamlaka ya sasa ya utafiti na ugani nchini Tanzania inapendelea zaidi mifumo ya kilimo cha kisasa na viwanda, kukuza kilimo cha kibiashara kutokana na kuimarisha ardhi na *wekevu wa mizani (kupungua gharama za wastani wa zao baada ya uzalishaji wa muda mrefu)*, na kujiunga na minyororo ya thamani dunia ambayo hunyonya rasilimali na utajiri kutoka kwenye bara.

Wakati tunaanza kujenga mawazo ya jinsi ya kufikiria upya ruzuku za kilimo kwa ajili ya wakulima wadogo, kuna vipengele vichache muhimu ambavyo vinaweza kuzingatiwa kuanzia mwanzo. Mwenyekiti wa Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) Mkutano wa Pili wa Kimataifa kuhusu Kilimo-Ekolojia, amependekeza kujenga mfumo ambao unaongozwa na familia na mkulima; na ***utafiti shirikishi na ubunifu wa pamoja*** ambao unazingatia watu, hujenga uwezo wa pamoja wa kutatua matatizo ya mfumo, unahimili tabia nchi, gharama nafuu, hukuza kujitegemea kwa maisha kwa familia za wakulima, unaweza kutumika na wenyeji, na hutumia rasilimali kwa uendelevu, na hubadilika kutokana na mrejesho (FAO, 2018).

Hii inaweza kujumuisha utafiti wa jambo halisi kulinganisha aina mbalimbali za mbegu zilizoboreshwa, mbegu za asili na aina za mkulima, kulingana na muktadha mahususi na utendaji. Inawezekana pia kujumuisha **kuendeleza aina za mbegu na wakulima kupitia ushirikishwaji wa kuzalisha mimea na ushirikishwaji wa kuchagua aina za mbegu**, ambazo zitaitikia maslahi na mahitaji yanayoingiliana ya wakulima (ACB, 2018). Jitihada kama hizi zitaweza kusaidia kutoa chaguzi kwa wakulima, kutunza na kuendeleza bioanuwai ya kilimo, na kuimarisha mifumo ya mbegu za wakulima na masoko ya ndani.

Hii inahitaji kwenda zaidi ya viashiria vya msingi vinavyotumika katika kutathmini aina na uwezo wao wa mavuno/hekta, kalori na kipato. Viashiria vinaweza kuongezwa na kujumuisha wigo mpana zaidi wa masharti ikiakisi mambo muhimu zaidi kijamii na kiekolojia kwa muda mrefu, kama vile:

- afya ya udongo hususani iliyopimwa kwa kuchambua virutubisho, kiwango cha

unyevunyevu, mabaki ya viumbe hai, na viumbe wakubwa na wadogo kwenye udongo;
- kiwango cha virutubisho/hekta;
- upatikanaji wa virutubisho na ubora wake;
- idadi ya uzalishaji/hekta;
- idadi ya viumbe vyote hai;
- ufanisi wa rasilimali;
- athari kwenye bioanuwai; utoaji huduma za mfumo wa ekolojia; na
- athari kwenye ustahimilivu wa maisha na usawa kijamii (IPES-Food, 2016).

***Miundo ya Kisheria na Udhibiti*** inapaswa kutoholewa kutoka mpito hadi kilimo-ekolojia ambayo inatokana na sera za chakula jumuishi na thabiti zinazohusisha sekta mbalimbali. Malengo na mipango ya muda mrefu yanayoheshimu haki za binadamu, hususani haki ya kupata chakula lazima iwe kiini. Kuhusiana na pembejeo kama vile mbegu, kuna haja ya kushughulikia ***Sheria za Mbegu*** za Tanzania na zile za ukanda mzima ambazo huzuia biashara, kubadilishana na mauzo ya mbegu ambazo hazijafuata masharti ya biashara. Ijapokuwa Mbegu za daraja la kuazimia (QDS) zinatambulika nchini Tanzania, mbegu kama hizo haziungwi mkono au kutumika kwenye programu za ruzuku za pembejeo. Mnamo 2015, wakati wa mchakato wa mapitio ya mbegu, mbegu za QDS zilipendekezwa kwa kupanuliwa hadi ngazi ya wilaya, ambayo ingefungua uwezekano kwa QDS kuwa na eneo kubwa zaidi la kijiografia (ESAFF, 2014; TOAM, 2015; ACB, 2016a). QDS inaweza kutoa fursa kwa uzalishaji wa aina za mbegu za mkulima, iwapo masharti ya kuwa ya kipekee, kufanana, na uthabiti wa mbegu (DUS) zitabadilishwa ili kuruhusu unyumbulishi zaidi kwa vifaa vya kuzaliana kulingana na aina za wakulima, na kujumuisha uchotara mkubwa zaidi. Hii ni muhimu kwa uhifadhi wa bioanuwai ya kilimo, uendelezaji na utohoaji unaochochea.

Kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uwezekano wa ***kusajili aina za mbegu asili za wakulima*** kunaweza kuchunguzwa na kushughulikiwa, kuelekea katika kutafuta njia zinazofaa ili kuhimili aina za mbegu za wakulima (SADC, 2008). SADC ina masharti ya kuweka lebo kwenye QDS kwa ajili ya biashara, ikiwa na dira ya kuhudumia mbegu za asili zilizosajiliwa. Masharti haya yafanyiwe uchunguzi kwa undani zaidi.

Kuna njia nyingi ambazo Serikali ya Tanzania inaweza kutumia programu hizi kusaidia na kuimarisha uzalishaji wa mbegu uliopo nchini, pia na mitandao ya mbegu ya wakulima. Wakulima na mashirika kama MVIWATA, Kilimo Endelevu Tanzania (SAT), Jukwaa la Wakulima Afrika Mashariki na Kusini (ESAFF), Matumizi Shirikishi ya Ardhi Kiekolojia (PELUM), Mtandao wa Bioanuwai Tanzania (TABIO) na Shirika la Kilimo Hai (TOAM) zinafanya kazi katika kuhifadhi, uchaguzi wa mbegu, na kuendeleza aina za mbegu, QDS na maeneo mengine. ESAFF, kwa mfano, imekuwa ikifanya kazi kuelekea kuthibitisha mbegu ya mahindi ya kienyeji chini ya masharti ya DUS, ili iweze kuingizwa sokoni.[7] Visa mkasa hivi hutoa uwezekano wa kujifunza kutokana na uzoefu huu wakati tukielekea katika kutafuta mifumo ya mbegu zinazofaa na stahiki kwa wakulima wadogo, na aina za wakulima.

Utendaji wa **Usimamizi jumuishi wa rutuba ya udongo** unatambulika na kipengele cha utendaji halisi ambacho kinaweza kujumuishwa katika kazi ya ugani. Kupanuka kwa Kilimo Hifadhi na Kilimo Kinachohimili Tabia-Nchi katika ukanda mzima na Tanzania (Rioux, 2017; Jayne, Sitko et al, 2018) kinafungua dirisha kuelekea mfumo wa uzalishaji wenye afya zaidi. Katika kiini chake, mbinu hizi zinatafuta kuboresha afya ya udongo kupitia utunzaji wa udongo. Mbinu za msingi ni kulima kidogo au kutokulima kabisa, mzunguko wa mazao/kilimo mseto, ardhi wakati wote kufunikwa na mimea kupitia kuweka matandazo na mazao ya jamii ya kunde yanayofunika ardhi. Kukuzwa kwa mbinu hizo ni hatua chanya.

Baadhi ya waungaji mkono wa Kilimo Hifadhi na Kilimo Kinachohimili Tabia-Nchi wanadai kuendelezwa kwa matumizi ya viua gugu na mbolea za viwandani. Wakati mwingine hoja ni kwamba kipindi cha mpito kinahitajika pale ambapo watu wamekuwa wakitumia pembejeo hizi. Hata katika maeneo mengine, kunaweza kuwepo kwa

7. Mahojiano na Mratibu wa Pelum Tanzania 24 Agosti 2017.

upungufu mkubwa wa virutubisho au tatizo la wadudu waharibifu, na kuna njia chache mbadala za kushughulikia tatizo hilo mara moja. Samadi ni nzito kusafirisha umbali mrefu na sio sehemu zote zina mifugo ya kutosha. Hata hivyo, ukiangalia nyuma ya Kilimo Hifadhi na Kilimo Kinahimili Tabia-Nchi msaada umeegemea zaidi kuelekea pembejeo za Mapinduzi ya Kijani, wakati rasilimali chache sana zimeelekezwa kwenye kujenga mbadala wa kilimo-ekolojia kwa kipindi kirefu. Kisiwa cha Mauritius kinatoa mfano wa nini kinaweza kufanyika. Kutokana na kiwango cha Mauri GAP[8] Ngazi 1, ruzuku za Serikali zinaelekezwa katika kutoa mbolea hai kwa wakulima.

Kwa sasa hata mbinu ya vocha ya kielektroniki humzuia mkulima katika kile kinachopatikana kwa wasambazaji wa pembejeo wanaoshiriki. Hii hubana kile kinachopatikana kwa wakulima. Pendekezo kutoka Ghana na Burkina Faso katika Afrika Magharibi ni kwamba wakulima wanapokea moja kwa moja motisha wa pesa taslimu kwa utendaji uliothibitika wa kilimo-ekolojia kama mbadala wa ruzuku za pembejeo za Mapinduzi ya Kijani.

Ijapokuwa ni katika mageuzi, programu za ruzuku za pembejeo ambazo zina asili ya siasa ya hali ya juu, hii inamaanisha haziwezi kusitishwa kirahisi namna hiyo. Hata hivyo, tunakoelekea sio bayana katika mwendelezo wa ruzuku za pembejeo, na hii ni fursa mwafaka kwa wakulima, Asasi za Kiraia na wengineo kupendekeza mifumo mbadala ya kuwasaidia wakulima ikijumuisha mbinu za anuwai wa kilimo-ekolojia.

7. Mahojiano na Mratibu wa Pelum Tanzania 24 Agosti 2017.
8. Kiwango cha MauriGAP Ngazi 1 ni kiwango cha msingi kwa uzalishaji wa mazao chini ya mifumo ya kilimo hai. Kiwango hiki tayari kimechapishwa katika Gazeti la Serikali. Lengo ni kuhimiza wakulima kuhama kutoka utendaji wa kilimo cha kawaida, ambacho kina misingi ya matumizi makubwa ya pembejeo za kemikali, hadi biokilimo au kilimo hai, kikiwa na matumizi kidogo au hakuna kabisa matumizi ya pembejeo za kemikali.

# Marejeo

ACB, 2016a. Changing seed and plant variety protection laws in Tanzania: Implications for farmer-managed seed systems and smallholder farmers. http://acbio.org.za/wp-content/uploads/2016/05/Tanzania-Seed-Law-2016.pdf

ACB, 2016b: Farm input subsidy programmes (FISPs): A benefit for, or the betrayal of, SADC's small-scale farmers? https://acbio.org.za/wp-content/uploads/2016/07/Input-Subsidies-Report-ACBio.pdf

ACB, 2018. A review of participatory breeding and lessons for African seed and food sovereignty movements. http://acbio.org.za/sites/default/files/documents/Full%20Report%20-%20English.pdf

Cagley JH, Gugerty MK and Plotnick R, 2009. Political Economy of Fertiliser Policy in Tanzania. Prepared for the Farmer Productivity Team of the Bill & Melinda Gates Foundation. Evans School of Public Affairs, University of Washington.

Cameron A, Derlagen C and Pauw K, 2017. Options for reducing fertilizer prices for smallholder farmers in Tanzania. Policy Report. Monitoring and analysing food and agricultural policies. Food and Agriculture Organization of the United Nations. http://www.fao.org/3/a-i7247e.pdf

DANIDA, 2012. Agricultural input subsidies in Sub-Saharan Africa. Evaluation Study 2011/12. https://www.oecd.org/derec/49231998.pdf

Demeke M, Spinelli A, Croce S, Pernechele V, Stefanelli E, Jafari A, Pangrazio G, Carracso G, Lanos B and Roux C, 2014. Food and agriculture policy decisions: Trends, emerging issues and policy alignments since the 2007/08 food security crisis. Food and Agriculture Organization of the United Nations. http://www.fao.org/docrep/019/i3514e/i3514e.pdf

ESAFF, 2014. Policy Brief on Seed. Need to improve access to quality seeds for small-scale farmers in Tanzania and other Eastern and Southern Africa Countries.

FAO, 2018. 2nd International Symposium on Agroecology: Scaling up agroecology to achieve the Sustainable Development Goals (SDGs); 3-5 April 2018, Rome. http://www.fao.org/3/CA0346EN/ca0346en.pdf

HLPE, 2013. Investing in smallholder agriculture for food security: A report by the High Level Panel of Experts on Food Security and Nutrition of the Committee on World Food Security, Rome. HLPE Report 6. http://www.fao.org/fileadmin/user_upload/hlpe/hlpe_documents/HLPE_Reports/HLPE-Report-6_Investing_in_smallholder_agriculture.pdf

IAASTD (International Assessment of Agricultural Knowledge, Science and Technology for Development), 2009. Agriculture at a crossroads: Global report. IAASTD https://www.globalagriculture.org/report-topics/about-the-iaastd-report.html

IAPRI (Indaba Agricultural Policy Research Institute) 2017. Achieving more with less: Reform and scaling down of FRA and FISP and boosting social protection. IAPRI Policy Advisory Paper. IAPRI, Lusaka.

IPES-Food, 2016. From uniformity to diversity: A paradigm shift from industrial agriculture to diversified agroecological systems. http://www.ipes-food.org/images/Reports/UniformityToDiversity_FullReport.pdf

Jayne, T., Mason, N., Burke, W. and Ariga, J. 2018. Taking stock of Africa's second-generation agricultural input subsidy programs. Food Policy, 75, pp.1-14. https://doi.org/10.1016/j.foodpol.2018.01.003

Jayne, T., Sitko, N., Mason, N. and Skole, D. 2018. Input subsidy programmes and Climate Smart Agriculture: Current realities and future potential, in L. Lipper et al. (eds), Climate Smart Agriculture, FAO Natural Resource Management and Policy 52. FAO, Rome.

Lim Li C, 2018. Agroecology for sustainable food systems. Environment and development series 19. Third World Network, Malaysia.

Mather D and Ndyetabula D, 2016. Assessing the drivers of Tanzania's fertilizer subsidy programs from 2003-2016: An application of the Kaleidoscope Model of policy chance. Feed the Future Innovation Lab for Food Security Policy, Research Paper 34.

Pan L and Christiaensen L, 2012. Who is vouching for the input voucher? Decentralized targeting and elite capture in Tanzania. World Development, 40(8):1619–33.

REPOA, 2017. Agricultural Policy Research 2015/16, National Agriculture Input Voucher (NAIVS) Implementation (draft). Dar es Salaam.

Rioux J, Laval E, Karttunen K, Lwakatare M, Natai S, Majule M, Massoy T, Malozo M and Bernoux M, 2017. Climate-smart agriculture guideline for the United Republic of Tanzania: A country-driven response to climate change, food and nutrition insecurity. Food and Agriculture Organization of the United Nations. http://www.fao.org/3/a-i7157e.pdf

Rodale Institute, 2011. The Farming Systems Trial: Celebrating 30 Years. http://rodaleinstitute.org/assets/FSTbookletFINAL.pdf

SADC, 2008. Technical agreements on harmonisation of seed regulation in the SADC region: Seed variety release, seed certification and quality assurance, quarantine and phytosanitary measures for seed. Gaborone, Botswana.

TOAM, 2015. Farmer managed seed systems in Tanzania. Operation, benefits, successes, challenges and support. http://www.kilimohai.org/fileadmin/01_images/Miscellaneous/TOAM_Seed_Book.pdf

URT (United Republic of Tanzania), 2012b. Ministry of Agriculture Budget Speech. http://www.kilimo.go.tz/uploads/Hotuba_11-07-2012_Final_Web.doc,

URT (United Republic of Tanzania), 2014a. Ministry of Agriculture Food and Cooperatives, Annual Report for fiscal year 2014/15. http://www.kilimo.go.tz/uploads/Annual_Report_2014_15_Final.docx

World Bank, 2014b. Implementation Completion and results report (IDA-46190, IDA-51730) on a credit in the amount of SDR 124.1million (US$ 185 million equivalent) to the United Republic of Tanzania for an Accelerated Food Security Project. Report number: ICR00003242. http://documents.worldbank.org/curated/en/132691468106739354/pdf/ICR32420P1142900disclosed0120300140.pdf

african centre for biodiversity

PO Box 29170, Melville 2109, South Africa
www.acbio.org.za